ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 28*** ***25th July, 2025***

## *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 27 Vol. 106 Dated 25th July, 2025*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 487 la tarehe 25/7/2025

SHERIA YA VYAMA VYA SIASA,
(SURA YA 258)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 22(2)(j))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KURATIBU MIKUTANO YA HADHARA YA VYAMA VYA SIASA ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 209 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Kuratibu Mikutano ya Hadhara ya Vyama vya Siasa za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Kuratibu Mikutano ya Hadhara ya Vyama vya Siasa, ambazo hapa zimerejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 5

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa-

(a) kufuta na kuandika upya aya (a) kama ifuatavyo:

"(a) jina, anwani ya makazi na namba ya simu iliyosajiliwa ya kiongozi wa chama;";

(b) kuongeza baada ya aya (a) aya mpya kama ifuatavyo:

(b) kitambulisho cha uraia, hati ya kusafiria, kitambulisho cha mpiga kura au leseni ya udereva ya kiongozi wa chama;"; na

(c) kubadili mpangilio wa aya (b) na (c) kuwa aya (c) na (d) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 8

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8 kwa-

(a) kubadili kanuni ndogo ya (1) kuwa kanuni ya 8;

(b) kufuta aya (g) na (h) na kuandika aya mpya ya (g) kama ifuatavyo:

“(g) kushawishi au kuchochea wanachama au wafuasi kufanya jambo lolote ambalo limekatazwa na sheria yoyote;”; na

(c) kubadili mpangilio wa aya (i) na (j) kuwa aya (h) na (i) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 9

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9 kwa kuongeza neno “ulemavu” baada ya neno “rangi” lililopo katika aya (a).

Dodoma,
23 Julai, 2025

WILLIAM V. LUKUVI
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu,*
*Sera, Bunge na Uratibu*